# Wabunge waingilia kati kupungua samaki Mtera

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji imewataka wavuvi katika Bwawa la Mtera kudhibiti uvuvi haramu kwa kuwa unasababisha kupungua kwa samaki kwenye baadhi ya maeneo.

Aidha, imeridhishwa na elimu iliyotolewa kuhusu uvuvi haramu kwa wavuvi hao.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dk. Christine Ishengoma, aliyasema hayo jana baada ya kufanya ziara katika kijiji cha Msisiri wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma na Kijiji cha Mnadani Wilaya ya Iringa na kuzungumza wavuvi na wananchi wa maeneo hayo.

Alisema katika vijiji vyote walivyopita wamekuta wavuvi na wananchi wanayo elimu hiyo na wanashiriki katika kudhibiti kwa kukamata nyavu haramu na kuziteketeza.

"Kwa kweli sisi kamati baada ya kuzungumza na wananchi pamoja na wavuvi wa maeneo yote hayo mawili tuliyotembelea tumeridhishwa na elimu iliyotolewa kuhusu uvuvi haramu kwa wavuvi wa Bwawa la Mtera," alisema.

Kadhalika, aliwaahidi wananchi wa Kijiji cha Mnadani kuwa atalifikisha tatizo la wingi wa viboko katika bwawa hilo kwa Waziri wa Maliasili na Utalii ili kulishughulikia.

Kwa upande wake, Katibu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Sekta ya Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, alisema wizara imekuwa ikitoa elimu kuhusu uvuvi haramu na madhara yake kwa wavuvi na wananchi wanaolizunguka bwawa hilo.

Alisema hatua hiyo imesaidia kudhibiti na kuteketeza nyavu zisizofaa zilizokamatwa.

Dk. Tamatamah aliwaahidi wavuvi wa kijiji cha Msisiri kuwaletea injini moja ya boti mwezi Julai, 2021 ambayo pamoja na shughuli za uvuvi itawasaidia kufanya doria za kudhibiti uvuvi haramu.

Aidha, alisema atatuma wataalamu wa utafiti kutoka TAFIRI kuangalia kutafiti kama upo uwezekano wa kuweka mbegu ya samaki ili kusaidia kuongeza wingi wa samaki kwenye bwawa hilo.

Aliwataka wavuvi kujiunga kwenye vyama vya ushirika ili kukopesheka na kupata zana sahihi za uvuvi zinazotolewa na wizara.

Naye Mkazi wa Kijiji cha Mnadani, Kata ya Izazi wilayani Iringa, Amiri Kiselo, aliiomba serikali kusaidia kukabiliana na ongezeko la viboko kwenye bwawa hilo ambao wanasababisha wavuvi kuhofia kuvua samaki.

"Tatizo hili limefanya samaki kuwa wachache katika masoko na kuwafanya wavuvi kutafuta shughuli nyingine za kuwaingizia kipato tunaomba kamati mtusaidie," alisema.

Scanned with CamScanner

KANDA Y

Mwanza, Geita, Simiy

Uk.11

# Wafugaji walalamikia vituo vya kuchenjulia dhahabu

**Na Yohana Shida, Geita**

BAADHI ya wafugaji wa ng'ombe na mbuzi wilayani hapa wamelalamikia uanzishwaji holela wa vituo na mitambo ya kuchenjulia dhahabu karibu na maeneo yao na kusababisha mifugo yao kufa kwa kula ama kunywa mabaki ya kemikali za uchenjuaji.

Wafugaji hao waliambia HabariLEO hivi karibuni kuwa, mitambo hiyo imegeuka kero na tishio kwao kwani wamiliki hawazingatii sheria ya mazingira kwa kutodhibiti vizuri kemikali ya sianidi ambayo ni hatari kwa mifugo.

Mmoja wa wafugaji hao, Iddi Mtasima mkazi wa mtaa wa Mbabani ata ya Mtakuja, alisema mifugo yake imeathirika na kemikali hiyo, hilo ambapo hivi karibuni ng'ombe wak mmoja alikufa kwa kunyw kemikali ya sianidi iliyokuwa imemwagwa kwenye shamba lake lilopo karibu na mtambo wa kuchenjulia dhahabu.

Mwenyekiti wa serikali ya mtaa wa Mbabani, Daudi Lupenda alisema iwapo hatua hazitachukuliwa kudhibiti tatizo hilo, mifugo itaendela kufa, kwani mwaka juzi alipoteza ng'ombe sita waliokufa kwa kunywa maji yenye mchanganyiko wa kemikali ya sianidi.

Ofisa Mifugo Kata ya Mtakuja, Swai Eben alisema amepokea malalamiko mengi ya wafugaji juu ya mifugo yao kufa baada ya kula na kunywa kemikali hizo.

Alisema ndani ya mwaka huu ameshapokea kesi zaidi ya 10 za ng'ombe na mbuzi kufa kwa kula kemikali hizo.

Ofisa Mazingira Ofisi ya Madini Mkoa wa Geita, Hussein Ally alisema kuna takribani vituo vya mitambo ya uchenjuaji 372.

Alisema kwa mjibu wa sheria ya usalama mahala pa kazi, wamiliki wanatakiwa kujenga miundombinu ya kuzuia muingiliano na jamii ikiwamo kujenga ukuta kuzunguka eneo la mitambo.

Scanned with CamScanner

Uk. 7

Na Gloria Tesha

# Serikali kudhibiti bei ya vifaranga, mayai

SERIKALI imesema itadhibiti bei holela ya mazao ya kuku kwa kuimarisha uwekezaji katika ufugaji wa mifugo hiyo na kuwakagua kwa kushtukiza wafugaji na kwenye mashamba ya kuku wazazi.

Aidha, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imesema, mwezi huu na Julai serikali imedhamiria kusiwe na uhaba wa vifaranga na hadi mwakani mwishoni kusiwe na uhaba wa kuku wazazi na mazao yake.

Wakati akiwasilisha bungeni bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema vituo vya kutotolesha vifaranga vimeongezeka kutoka 26 mwaka 2019/2020 hadi 28 hivi sasa.

Alisema vituo hivyo vipo katika mikoa ya Dar es Salaam (9), Pwani (11), Iringa (2), Arusha (1), Kilimanjaro (2), Mbeya (1), Mwanza (1).

Aliwaeleza wabunge kuwa kati ya mwaka 2019/2020, mashamba ya kuku wazazi yaliongezeka kutoka 20 hadi 22 na yana uwezo wa kutunza kuku wazazi 1, 300,000. Mashamba hayo yanazalisha kuku wa nyama, kuku wa mayai na chotara.

Ndaki alisema kuku wa asili wameongezeka kutoka milioni 38.77 hadi milioni 40.36 na kuku wa kisasa wameongezeka kutoka milioni 44.51 hadi milioni 47.34.

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Hezron Nonga, alisema ufugaji kuku ni muhimu katika ukuaji wa pato la taifa kwa kuwa kati ya asilimia 7.4 inayochangiwa na sekta ya mifugo, asilimia 1.8 inatoka kwenye ufugaji wa kuku.

Alilieleza HabariLEO kuwa, wizara imebaini changamoto kadhaa zinazofifisha ukuaji huo zikiwemo hujuma zinayofanywa na baadhi ya wafugaji wa kuku wanaotengeneza uhaba wa mazao ya kuku.

Pia alisema wizara inazifahamu changamoto zinazowakabili wafugaji ukiwemo ufuatiliaji wa chanjo kwa uhakika, vyakula vyenye ubora na wengine wakikimbilia kuuza kuku wakiwa bado wadogo.

"Sekta hii ni muhimu sana kwani katika kaya milioni 10 zinazofuga wanyama mbalimbali nchini, zaidi ya kaya milioni tano wanafuga kuku (wa kienyeji na wa kisasa), lakini wafugaji wengi wa kuku hawana vyama jambo linalodumaza sekta ya ufugaji wa kuku," alisema Profesa Nonga.

Aliwahimiza wananchi kufuga kuku na kwamba kwa sasa kuku wa nyama ni wengi zaidi na hukuzwa kwa wiki sita hadi saba na kuchinjwa.

"Huyu wa mayai anataga kwa miaka miwili. Kiwango ni kidogo, tamanio ni tuwe na kuku wa mayai zaidi ya milioni 20 kutoka vifaranga vya mayai milioni 7.384," alisema Profesa Nonga.

Alisema serikali inatamani nchi iwe na vifaranga vya kuku wa mayai zaidi ya milioni 20 hivyo Watanzania wachangamkie fursa hiyo.

Ndaki alisema bungeni kuwa, katika mwaka 2020/2021, vifaranga 88,348,000 vimezalishwa na kusambazwa nchini.

Alisema kati ya hivyo, vifaranga 52,000,000 ni wa nyama, vifaranga 28,964,000 ni vya kuku chotara ambapo Sasso ni 15,600,000 na Kroiler 13,364,000 na vifaranga 7,384,000 ni wa kuku wa mayai.

"Katika mwaka 2021/2022, wizara itaendelea kushirikiana na wazalishaji wa vifaranga vya kuku ili kuhakikisha wafugaji wanapata vifaranga bora katika ukuaji na ustahilivu wa magonjwa ili kujikomboa kiuchumi,"alisema Ndaki.

Profesa Nonga alisema uhaba uliosababishwa na janga la corona sasa unakwisha na alizitaka kampuni zilizosajiliwa ziombe kibali cha kufungua mashamba ya kuku wazazi.

Alisema kuna changamoto ya uzalishaji wa bidhaa za kuku hivyo wafugaji waanzishe vyama ili kuzitatua changamoto kwa pamoja.

Profesa Nonga alisema sasa kuna utoaji wa vibali vya kuingiza nchini kuku wa nyama tofauti na zamani viliporuhusiwa vya vifaranga vya kuku wazazi pekee.

Alisema wizara inafahamu mashamba 28 ya kuku wazazi hayatoshelezi hivyo kampuni zilizosajiliwa ziombe vibali vya kuyaanzisha.

Mikoa inayoongoza kwa wingi wa kuku wa kienyeji na asilimia zake kwenye mabano ni Tabora (6.5), Mwanza (5.2), Shinyanga (5.2), Morogoro (5.1), Geita (5.1) na Dar es Salaam (4.5).

Scanned with CamScanner